

TANGAZO LA SERIKALI Na. 298 la tarehe 7/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURA YA 355)

AMRI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))

AMRI YA KUPANGA ENEO LA KATOMA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Katoma ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango ya Jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali inaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Mji wa Geita.

JEDWALI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo-

“Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira – nukta 413994MS, 9682314KZ kwa umbali wakilometa 0.36 kuelekea Nyanza hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 413731MS, 9682569 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa 153⁰ kwa umbali wa kilometa 0.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba Cyenye majira - nukta 413443MS, 9682659KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa 137⁰ kwa umbali wa kilometa 0.15 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 413310MS, 9682595KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa 90⁰ kwa umbali wa kilometa 0.67 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira nukta 413264MS, 9683268KZ; baada ya hapo mpaka unafuata hifadhi ya msitu wa Geita katika uelekeo wa 134⁰ kwa umbali wa kilometa 0.74 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba Fyenye majira - nukta 412542MS, 9683214KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini- Magharibi kwa umbali wa kilometa 0.56 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G yenye majira - nukta 412180MS, 9682781KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa 111⁰ kwa umbali wa kilometa 0.45 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H yenye majira- nukta 412399MS, 9682393KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa 154⁰ kwa kufuata mtaa wa Kompaund kwa umbali wa kilometa 0.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba I yenye majira - nukta 412411MS, 9682189KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa 87⁰ kwa umbali wa kilometa 0.26 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba J yenye majira - nukta 412656MS, 9682283KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa 88⁰ hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ‘K’ yenye majira - nukta 412839MS, 9681712KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa 166⁰ kwa umbali wa kilometa 0.53 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba L yenye majira – nukta 413342MS, 9681890KZ; baada ya hapo mpaka unafuata mpaka wa mtaa wa Lwenge kwa umbali wa kilometa 0.78 hadi ulipoanzia”

Dodoma,
17, Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na
Maendeleo ya Makazi*